

Rasilimali za Jinsi ya Kupata Uuguzi wa Kiafya kwa Bei Nafuu au kupata Bima ya Afya

Kupata huduma ya afya kwa bei nafuu

- **Bridge to Benefits: Orodha ya kutoa huduma ya afya kwa bei nafuu MN**
(www.bridgetobenefits.org/MN_Low_Cost_Health_Care_Directory)
Weka kata yako ili kupata orodha ya kliniki za bei nafuu zilizo karibu nawe.
- **Minnesota Association of Community Health Centers (MNACHC) (Jumuiya ya Vituo vya Afya ya Jamii ya Minnesota (MNACHC))**
(<https://mnachc.org/community-health-centers/find-a-health-center/>)
Tumia ramani au uweke eneo ili kupata Kituo cha Afya ya Jamii (Kituo cha Afya cha Kiwango cha Serikali Kuu) kilicho karibu nawe. Vituo vya Afya ya Jamii hutoa huduma za afya za kimatibabu, meno, na tabia kwa watu wenye ufikiaji mdogo wa utunzaji.

Pata bima ya afya

- **MNSure Apply and Enroll for insurance (MNSure Tuma maombi na Usajiliwe kwenye bima)**
(www.mnsure.org/new-customers/apply/index.jsp)
Unaweza kutuma ombi la kusajiliwa kwenye bima, kama vile Medical Assistance na MinnesotaCare, mtandaoni au kupata mtaalamu wa usajili akusaidie. Wakaazi wengi wa jimbo la Minnesota wanaojisajili kupitia MNSure wanastahiki msaada wa kifedha.
- **MNSure Navigators (Wataalamu wa Usajili wa Mnsure)**
(<https://www.mnsure.org/help/find-assister/find-navigator.jsp>)
Wataalamu wa usajili wanaweza kukusaidia kujisajili kwenye Medical Assistance au MinnesotaCare (ikiwa unastahiki). Wanaweza pia kukusaidia kujisajili katika mpango wa bima ya kibinafsi na kutoa elimu ya msingi ya bima ya afya. Wataalamu wengi wa usajili wanapatikana kwenye mashirika ya jamii na hutoa usaidizi kwa lugha mbalimbali ikiwemo Kichina, Kisomali, Kihispania, Hmong na Kivietnamu.
- **Hospital Presumptive Eligibility Program (Mpango wa Kudhaniwa Kustahiki ukiwa Hospitalini)**
(<https://mn.gov/dhs/partners-and-providers/policies-procedures/minnesota-health-care-programs/provider/hpe/>)
Huenda ukaweza kujisajili kwa Medical Assistance au MinnesotaCare unapokuwa hospitalini. Ikiwa unatimiza mahitaji, unaweza kugharimiwa na bima kabla ya kukamilisha ombi kamili.

Pata huduma za ziada za afya

- **Idara za Afya za Eneo Husika na Bodi za Afya ya Jamii**
(<https://www.health.state.mn.us/communities/practice/connect/findlph.html>)
Wasiliana na idara ya afya ya eneo husika na/au bodi ya afya ya jamii katika kata yako ili kupata mwongozo na kuuliza kuhusu huduma ambazo huenda unastahiki.

Minnesota Department of Health
625 Robert St. N., PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-5414
www.health.state.mn.us

2/13/2020

Ili kupata taarifa hii katika umbizo tofauti, piga simu kwa: 651-201-5414.